AFRICAN CLEAN CITIES PLATFORM
PLATE-FORME AFRICAINE DES VILLES PROPRES
UN-HABITAT
WASTE WISE CITIES

# TAKA LANGU, UKWASI WETU


—

CHANGIA KUPATA SULUHISHO!




Mwanangu, tafadhali nenda utenganishe taka. Watoza takataka watakuja kesho.
Siwezi weka kila kitu katika pipa moja? Kwanini lazima nitenganishe?


Hilo ni swali nzuri sana. Ikiwa tutatenganisha, itakuwa inawezekana kuchakata taka. Hii inaokoa rasilimali yetu asili. Wakati huo huo inazalisha mengine mapya.
Kweli? Hiyo inawezekanaje?
Plastiki, karatasi na glasi zikikusanywa kando, zitakuwa safi kutoka mabaki ya chakula, kwa hivyo rasilimali kiasi itahitajika kuzibadilisha ziwe vitu vipya.


Kwa mfano, taka za chakula zikikusanywa kando, zitabadilishwa kuwa mbolea ya kikaboni, biogas au umeme.
Kutenganisha taka husaidia kuunda kazi mpya na kutengeneza mapato na maisha bora pia!
Kwa kuchagua taka, tunaweza kutoa nishati safi pia!


Sawa...
Lakini nini itatokea ikiwa sitatenganisha taka?
Taka iliyochanganywa huishia kwa tovuti za taka ambazo huchangia uchafuzi wa maji, udongo na hewa. Ni muhimu kwetu kukuza afya ya mazingira yetu ili itupe chakula, maji na hewa tunayohitaji katika maisha yetu.
Sitaki kukaa bila chakula au maji, kwa hivyo nataka kulinda mazingira yetu! Nini kingine ninachoweza kufanya?



Katika shule, nilijifunza kuhusu 5Rs! Rethink, Refuse, Reduce, Reuse, Recycle.
Asilimia kubwa ya vitu tunavyotupa sio taka bali ni rasilimali (RETHINK).




Tunaweza tumia tena (**RE-USE**) hii chupa ya glasi mara nyingi kwa kuhifadhi maji ama tukikiweka kwenye pipa tofauti, kampuni za kuchakata zinaweza kukitumia kutengeneza vitu vipya vya glasi




Jambo lingine muhimu unaweza kufanya ni kuvikataa (**REFUSE**) vitu vya matumizi moja...




Hivi ni vitu unazotumia mara moja tu, mara nyingi tu dakika chache kisha kutupa... Kwa mfano, plastiki nyavu ya mboga na matunda.






Ahh, naelewa sasa. Ninaonanga nyavu hizi kila wakati tunapoenda kununua chakula. Tunazitumia kubebea chakula kisha tunazitupa.
Wakati mwingine tutumie mifuko tunayoweza tumia mara nyingi ndio tusiongeze taka.


Reuse husaidia kuokoa rasilimali na kulinda mazingira yetu pia.
Kwa mfano, wakati binamu wenu wakubwa huwapa nguo ambazo haziwatoshi...
Unaweza kupeana vitabu au vifaa vya kuchezea ambavyo hautumii kama zawadi. Kuwa mkarimu kwa marafiki zako, familia na  sayari yetu!


Wakati mwingine tunataka vitu vipya ingawa hatuvihitaji
tunahitaji kufikiria mara mbili kabla kununua chochote...
Njia bora zaidi ya kusimamia taka ni kutozizalisha!Kwa njia hiyo tunapunguza (Reduce) taka kizazi.
Vipi kuhusu R ya mwisho?
Recycling! Angalia t-shati yako: unajua kuwa imetengenezwa kutumia vyupa vya plastiki vya zamani?
Teknolojia na uvumbuzi unaweza kutusaidia kulinda mazingira yetu!



Angalia ni kiasi gani taka zetu zimepunguzwa kutumia 5Rs.
Sasa, hii taka pekee itaenda kutupwa... zingine zitaokolewa.
KARATASI
PLASTIKI
KIOO
CHUMA
TAKA HAI


Kuna msemo:
Taka ikichanganywa, rasilimali ikitenganishwa!
Tunapunguza taka na kuokoa rasilimali na nyenzo mbichi kwa kuzijitenganisha!


Nitajaribu kulinda mazingira yetu na kuzalisha utajiri kwa jamii yetu kutumia 5Rs! Ikiwa bado ninayo taka, nitahakikisha imewekwa mahali inayofaa.
Hiyo ndio njia! Kila mtu hutoa taka, kila mtu ana jukumu kwa hiyo taka na kila mtu anaweza kufaidika nayo!


Unakimbilia wapi?
Nataka kuambia rafiki zangu kuhusu 5Rs! Pamoja tunaweza kufanikiwa zaidi!
SHUJAA WA TAKA



**KWA MAELEZO ZAIDI KUHUSU JINSI YA KUCHUKUA HATUA ILI KUBORESHA UDHIBITI WA TAKA NGUMU WA MANISPAA KATIKA MIJI NA JUMUIYA ZAKO.**

## TUTEMBELEE KWA

[HTTPS://UNHABITAT.ORG/WASTE-WISE-CITIES](https://unhabitat.org/waste-wise-cities)

[HTTPS://AFRICANCLEANCITIES.ORG](https://africancleancities.org)

**SHIRIKI NASI MIKAKATI YAKO YA UHAMASISHAJI NA UHAMASISHAJI:**

- UMEFANIKISHA NINI?
- CHANGAMOTO ZIPI UMEKUTANA NAZO?
- JE, UMEZISHINDA VIPI?

## TUAMBIE KWA

WASTEWISECITIES@UN.ORG

ACCP@UN.ORG



AFRICAN CLEAN CITIES PLATFORM
PLATE-FORME AFRICAINE DES VILLES PROPRES

UN-HABITAT

WASTE WISE CITIES